# Mpango wa Kupimwa na Kukaa
# Maswali Yanayoulizwa Mara na Mara

## 1. Kupimwa na Kukaa (Test to Stay) ni nini?

Kupimwa na Kukaa ni itifaki mpya inayojaribiwa katika Shule za Umma za Kata ya Fayette (FCPS), kwa kushirikiana na Idara ya Afya ya Kentucky (KDH), Idara ya Afya ya Kata ya Lexington-Fayette (LFCHD), na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa vya Merika (CDC). Ni dhana mpya iliyotabiriwa juu ya data ambayo inaonyesha wanafunzi wengi ambao wanapimwa na kupatikana na virusi vya COVID-19 toka mazingira isiyohusiana na shule. Mpango huu, kama jina lake linavyosema, unaruhusu wanafunzi kuchukua vipimo ya mara kwa mara ili wabaki shuleni na katika majifunzo ya kibinafsi, ambayo tumeona ndio bora kwa wanafunzi.

## 2. Nilidhani watu wanaweza tayari kupimwa kutoka kwa karantini (kitengo)?

Tunao mpango ambao unaruhusu wanafunzi kufupisha kipindi cha karantini kwa kupimwa siku ya tano, sita, au saba baada ya kutengwa ili warudi shuleni siku ya nane ikiwa kipimo chao hakina virusi. Mpango huo bado unaomba wanafunzi wabaki nyumbani na mbali ya mazingira ya shule kwa siku saba.

## 3. Je! Itifaki hii ina utofauti gani?

Wanafunzi waliotambuliwa kwa kujitenga ambao hawana dalili zozote za COVID-19 watapimwa shuleni siku za Jumatatu, Jumatano, na Ijumaa hadi siku saba baada ya kuwa na mahusiano ya karibu na mgojwa. Ikiwa kipimo chao hakina virusi, wanaweza kuendelea na darasa. Ikiwa kipimo chao kina virusi, watahitaji kurudi nyumbani na kujitenga.

## 4. Kwa hivyo, wanafunzi katika mpanog huu hawaitaji kujitenga kabisa?

Kwa kweli, bado wako karantini. Ila, inamaanisha, kwa mda wa siku saba, hawapaswi kwenda mahali pengine popote bali shuleni, ili kupimwa, kuhudhuria darasa na kurudi nyumbani.  Kusudi ni kuzuia uenezi wa virusi katika jamii.

## 5. Je, itifaki hii ni kwa wanafunzi na wafanyikazi pekee?

Hapana, mpango huu ni kwa wanafunzi tu. Watu wazima wanastahiki chanjo, wakati wanafunzi wengi hawastahili. Watu wazima ambao hutambuliwa kama mawasiliano ya karibu na hawajachanjwa watahitaji kutengwa nyumbani, wakitumia wakati wao wa likizo.

## 6. Je! Familia zitahitaji kutoa kadi ya bima ya afya au kulipia vipimo?

Hapana, vipimo vinatolewa kwa shule kupitia ruzuku (msaada wa kifedha) toka serikali. Walakini, familia lazima zitowe idhini (ruhusa) ya vipimo, hazitaulizwa kutowa maelezo ya bima ya afya au ya bili.

## 7. Je! Hii itafanyika vipi?

Wanafunzi wanaotambulika kuwa mawasiliano ya karibu na mgonjwa watapokea habari juu ya mpano huu na fomu ya idhini ya kurudisha shuleni. Katika kipindi cha kujitenga watakuja mahali pa kupima (kwa kawaida ni eneo la mazoezi au kahawa ya shule) Jumatatu, Jumatano na Ijumaa na kusubiri kupimwa. Vipimo vinavyo tumiwa ni vipimo vya haraka PCR ambavyo vinatowa jibu baada ya dakika 30-45. Mara tu matokeo yanapojulikana, wanafunzi ambao majibu haina virusi wataendelea darasani. Wale ambao majibu ina virusi watarudishwa nyumbani na watahitaji kujitenga kwa muda wote ambao wanaweza kuambukiza.

## 8. Je! Nitahitaji kufuatilia wanafunzi katika darasa langu?

Hapana, tuna rasilimali shuleni ambayo itashughulikia habari muhimu za kufuatilia (contact tracing). Watasaidiwa na kampuni ya kufanya vipimo na watu kutoka CDC, ambao watasaidia katika kurahisisha mchakato.

## 9. Je! Hii itazuiya vipi uenezi wa virusi?

CDC, Idara ya Afya ya Kentucky, na Idara ya Afya ya Kata ya Lexington Fayette wamekuwa wakifuatilia kesi kwa miezi 18 sasa.  Na walitambuwa kwamba hatari ya mahambukizi shuleni ni duni (iko chini). Kesi nyingi za wanafunzi wenye virusi zatoka kwa kesi zilizo katika familia zao au kupitia mawasiliano ya kijamii, na sio ndani ya darasa lao.

## 10. Je! Wanafunzi ambao wanahitaji kujitenga kwa sababu mwanamemba wa familia ameonekana kuwa na ugonjwa wa COVID-19 wataweza kushiriki?

Hapana. Wanafunzi wengi wanapata COVID-19 baada ya kuwasiliana katika mazingira yao ya nyumbani. Kwa hivyo, wanafunzi ambao wana mwanafamilia aliye na COVID-19 wataendelea kutengwa na Idara ya Afya kwa siku 10-20 kulingana na hali.

## 11. Je! Wilaya pia itahimiza “Kupimwa na Kucheza” kwa timu za michezo na shughuli za zaidi ya mitaala (extra-curricular activities)?

Lengo letu ni kuongeza muda wa kufundisha. Wanafunzi wa shule zilizo katika mpango hu una ambao wanakabiliwa na COVID-19 kwa sababu yoyote inayohusiana na shule – ikiwamo kushiriki katika shughuli za riadha na za ziada za masomo - wana fursa ya kushiriki katika mpango wa Kupimwa na Kukaa na wanaweza kuhudhuria shule na kuendelea na shughuli hizo ikiwa watabaki bila dalili na vipimo vikiwa vizuri. Walakini, hakuta kuwa vipimo pekee kwa timu za michezo na kwa shughuli za baada ya shule.

## 12. Kwa hivyo, mpango huu ukiwepo, je, tunaweza kurudi kwa jinsi mambo yalikuwa kabla ya COVID?

Hapana. Bado tutahitaji kuweka wanafunzi kwenye vikundi (cohorts), kudumisha chati za kukaa, na kufuatilia mawasiliano na harakati za wanafunzi katika jengo lote kwa sababu za kufuatilia mawasiliano. Mpango huu unapunguza tu idadi ya siku za kufundisha ambazo mwanafunzi amekosa, sababu inaruhusu wanafunzi kubaki shuleni, ikiwa hawana dalili za COVID-19 na ikiwa vipimo vyao kila siku ya kujitenga havionyeshe virusi.

## 13. Je! Ikiwa familia inaamua kutoingia kwenye mpango huu na kisha kubadilisha mawazo yao?

Familia haiwezi kuchagua kuingia au kutoka kwenye mpango wa Kupimwa na Kukaa wakati karantini imeanza. Ikiwa wataamua kupimwa, watahitaji kupimwa kila siku iliyopangwa ili kubaki shuleni, AU ikiwa wataamua kujitenga, wanawezi kuja shuleni hadi karantini yao imekamilika. Njia yoyote watakayofuata siku ya kwanza, itakuwa njia yao hadi mwisho wa kipindi cha karantini.

## 14. Itakuwa je wikendi na siku za likizo?

Kwa kuwa vipimo vya mpango huu havifanyiki wikendi au siku ya likizo, wanafunzi watajitenga nyumbani na kupimwa siku ya vipimo inayofuata.

## 15. Je! Ikiwa wanafunzi wanafika chelewa shuleni?

Tutakuwa na idadi ndogo ya vipimo vya haraka vya antigen ambavyo tunaweza kutimia kwa wanafunzi wanaofika chelewa baada ya saa za vipimo. Aina hii ya vipimo itatumiwa marahaba tui li kusaidia mwanafunzi abaki shuleni.

## 16. Kwa nini shule zote haziwezi kushiriki?

Kama tulivyoonyesha, tunajaribu mpango huu kwa kushirikiana na CDC ili kuhakikisha ikiwa itapanuliwa hadi maeneo mengine ya shule.

## 17. Je! Shule zilichaguliwaje?

Tulichagua shule ambazo zilikuwa na idadi kubwa ya kesi za COVID-19 na karantini wakati tulianza mpango. Tulijaribu pia kuchagua shule katika maeneo tofauti ya mji, ili kupata sampuli nzuri ya idadi ya watu. Mpango huo ni wa shule za msingi na za kati hivi sasa, kwa sababu wanafunzi wengi katika majengo hayo hawastahiki chanjo. Kwa ngazi ya shule ya upili (sekondari), wanafunzi wana fursa ya kupata chanjo ili wasilazimike kujitenga isipokuwa wataonyesha dalili za COVID-19.